# TATHMINI YA MADARASA YA JUU YA DISTINCTION

## MONITORING LEARNER'S PROGRESS

## GREDI YA SITA - 2026

## SHUGHULI ZA KISWAHILI

6

PREMIER

QUALITY IS OUR CONCERN 001

*saa moja na nusu*

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1 hadi 5**

**Daktari:** Habari za alasiri binti? Karibu sana kwenye hospitali ya Tiba bora.

**Nyambura:** Sijambo daktari. Nimekutembelea kwa sababu sihisi vyema kabisa kwenye mapafu yangu.

**Daktari:** Maskini! Pole sana kwa jinsi unavyosikia. Unahisi vipi? Umeanza kuhisi hivyo tangu lini?

**Nyambura:** Nimekuwa na maumivu makali ya mapafu, ninapopumua usiku napata shida sana. Muda mwingine nahisi baridi na uchungu hasa ninapokohoa.

**Daktari:** Pole sana binti. Nitakuchunguza kisha niweze kutambua hasa chanzo cha hali yako. Usiku huwa unahisi joto?

**Nyambura:** Naam, huwa ninapata joto jingi usiku. Isitoshe, kuna muda nahisi uchovu mwingi mwilini.

**Daktari:** Haya hebu nikupime joto kisha niangalie mapigo ya moyo. Inaonekana kifua chako ili tujue hali halisi.

**Nyambura:** Naweza kuwa na kifua kikuu?

**Daktari:** Sina hakika, tusubiri kwanza tufanye vipimo kisha tutajua ukweli. Vipimo hivi vitatufahamisha ni nini hasa kinachokuuma kisha tutaweza kukutibu.

**Nyambura:** Shukran sana daktari. Nimeshukuru kwa wema wako.

**Maswali.**

1. Nyambura alienda hospitalini wakati gani wa siku?
   A. Baada ya adhuhuri
   B. Kabla ya alfajiri
   C. Muda wa asubuhi
   D. Mwendo wa machweo
2. Mapafu hufanya kazi gani katika mwili wa binadamu kulingana na mazungumzo haya?
   A. Husafisha damu
   B. Husafisha hewa
   C. Husaga chakula
   D. Hudhibiti viwango vya sukari
3. Mtu akikuambia pole unafaa kumjibu kwa kusema vipi?
   A. Pole pia B. Karibu
   C. Pole haiponyi D. Nimeshapoa
4. Mtu akitaka kupima kiwango cha joto katika mwili anatumia kifaa gani?
   A. Stethoskopu B. Kipimajoto
   C. Sirinji D. Kitata
5. Unadhani mazungumzo haya yanaendelea katika sehemu gani ?
   A. Shuleni B. Hospitalini
   C. Dukani D. Sokoni

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 6 hadi 10.**

Umaskini ni hali ya kukosa mali au pesa ambayo inampelekea mtu kukosa kuweza kukidhi mahitaji yake ya kimsingi pamoja na ya wale ambao wanamtegema. Hali hii humfanya mtu akose kuwa na mavazi mazuri, chakula cha kutosha, makazi na hata kukosa kujiendeleza kielimu. Mtu ambaye ni maskini huwa hana uwezo wa kujiamulia mambo mengi hasa yanayohitaji uwezo wa fedha.

Mtu anaweza kujitoa katika hali ya umaskini kwa kufanya biashara akitumia pesa na baadaye apate faida. Faida hutumiwa kununua na kulipia bidhaa muhimu katika maisha. Hata hivyo, ikiwa mtu huyo hatatumia pesa vizuri, anaweza kupata hasara.

Mbali na biashara, mtu anaweza kusoma na kupata ujuzi ambao utampatia ajira na njia za kujitegemea mbeleni. Akiwa kazini anaweza kulipwa mshahara mwishoni mwa mwezi. Malipo haya anaweza kuyatumia kulipia gharama za maisha pamoja na kujiwekea akiba kidogo. Akiba humsaidia mtu wakati ambapo ameishiwa na kipato na kuna dharura.

Baadhi ya watu hujihusisha katika kilimo. Wanaweza kupanda mazao ama kufuga wanyama kama vile ng'ombe na mbuzi na kupata faida kemkem. Wanyama hawa huuzwa na kuleta faida kwa wafugaji. Ni vyema kila mmoja kushiriki katika shughuli za kiuchumi ambazo zinasaidia kupiga teke umaskini na kumfanya kila mmoja kuweza kuishi maisha yanayostahili.



CamScanner

**Maswali.**

6. Kulingana na ufahamu ni kweli kusema kuwa.
   A. Kila mtu asiyekuwa na mali mengi hana chakula na mavazi
   B. Masikini huwa hawawezi kupata mali na pesa
   C. Mtu asiyekuwa na mali na pesa hupata huduma za kimsingi kwa shida
   D. Masikini wengine wana mali na pesa lakini hawana elimu
7. Watu wanaotumia pesa zao vizuri katika biashara huenda wakapata nini?
   A. Faida B. Bidhaa
   C. Hasara D. Mtaji
8. Kifungu kinasema kuwa masomo yanaweza kumpatia mtu nini?
   A. Pesa za kufaulu katika maisha
   B. Faida katika biashara
   C. Hasara ikiwa biashara haitafanikiwa
   D. Ujuzi wa kuweza kujitoa katika umskini
9. Mtu akiishiwa na pesa zake ama awe na dharura anaweza kupata msaada kutoka kwa.
   A. Marafiki B. Akiba
   C. Mshahara D. Serikali
10. Ni ipi miongoni mwa hizi si shughuli ya kiuchumi ambayo inaweza kumfaa mtu?
    A. Kufuga mifugo
    B. Kupanda mazao na kuyauza
    C. Kupata ajira
    D. Kutamani pesa

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo kutoka 11 hadi 15.**

Leo nawaelezeni, msikilize vizuri,
Nisemayo yashikeni, nataka niyakariri,
Wa bara na hata mijini, nawaeleza dhahiri,
Mazingira tuyalinde, yasichafuke daima.

Mito yetu kuchafua, si jambo lenye faida,
Mito ni maji tambua, kesho tusilete shida,
Maziwa yetu na mvua, tulinde kaka na dada,
Mazingira tuyalinde, yasichafuke daima.

Mwisho ninamalizia, hewa nayo tuitunze,
Misitu na miti pia, kuitunza tujifunze,
Udongo unapopitia, usiende tuukinze,
Mazingira tuyalinde, yasichafuke daima.

**Maswali.**

11. Shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti kama hili huitwa?
    A. Tathlitha B. Takhmisa
    C. Tarbia D. Tahnia
12. Mshairi anazungumzia jambo gani katika shairi hili?
    A. Umuhimu wa maji
    B. Umuhimu wa kutunza mazingira
    C. Umuhimu wa mashairi
    D. Umuhimu wa beti
13. Kibwagizo cha shairi hili kinasema kuwa
    A. mazingira tuyalinde, yasichafuke daima
    B. mwisho ninamalizia, hewa nayo tuitunze
    C. leo nawaelezeni, msikilize vizuri
    D. mito yetu kichafua, si jambo lenye faida
14. shairi hili lote lina mishororo mingapi?
    A. kumi na mitano
    B. kumi na miwili
    C. kumi na minane
    D. kumi na sita
15. Ni sehemu gani ya mazingira ambayo haijatajwa na mshairi?
    A. maji B. hewa
    C. madini D. misitu



CamScanner

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo kutoka 16 hadi 20.**

Fatuma Bahati __16__ mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na __17__ katika Kijiji cha Majimarefu. Alijiunga _18_ shule ya msingi ya Bidii. Baada ya shule ya msingi, alijiunga na shule ya upili ya Ufanisi. Aliendelea na masomo yake hadi _19_daktari.Alipohitimu, alirudi kijijini kwao na kuwasaidia wanajamii. Alianza kampeni ya kuwaelimisha wanakijiji kuhusu umuhimu wa usafi wa mwili na _20_.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 16 | A. alizaliwa | B.angezaliwa | C.amezaliwa | D.atazaliwa |
| 17 | A.tisini | B.kenda | C.korija | D.sabini |
| 18 | A.pamoja | B.kwa | C.kwenye | D.na |
| 19 | A.akabadilika | B.akawa | C.akakuwa | D.akaingia |
| 20 | A.mazingara | B.masingara | C.mazingira | D.masihara |

**Kutoka swali la 21 hadi 30, jibu swali kulingana na maelekezo.**

21. Ukubwa wa **kisu** ni **jisu**, kama vile ukubwa wa **kioo** ni
    A. choo
    B. joo
    C. jioo
    D.jikioo

22. Kanusha sentensi ifuatayo. Ukifika utapata zawadi yako.
    A. usingefika usingepata zawadi yako
    B. hukufika wala hukupata zawadi yako
    C. ukifika hautapata zawadi yako
    D. usipofika hautapata zawadi yako

23. Tambua kinyume cha neno lililopigiwa mstari. Makuli **wanapakia** mizigo kwenye meli.
    A.wanaondoa
    B.wanapakua
    C.wanapangia
    D.wanaepua

24. Ni nomino gani ambayo haipatikani katika ngeli ya YA-YA miongoni mwa hizi?
    A. maji
    B.maisha
    C.maradhi
    D. mabao

25. Ni sentensi ipi ambayo imeakifishwa kwa usahihi?
    A.Meli kubwa imeng'oa nanga bandarini.
    B. Jamani, naomba tushirikiane kumbeba mgonjwa!
    C.Nimeona ndege wa kupendeza katika ziwa nakuru
    D.Nimenunua; viazi, mihogo,tomato na vitunguu.

26. Ni sentensi gani yenye kivumishi kiashiria kati ya hizi?
    A. Kamba ndefu iliyomfunga mbuzi ni yangu.
    B.Afisa huyo alitufundisha kuyatunza mazingira.
    C. Mkoba wangu umetoboka tukitoka sokoni.
    D. Kisu chenyewe kimenolewa na mpishi.

27. Ni sentensi ipi iliyoandikwa katika nafsi ya pili umoja?
    A.Wewe utaimba wimbo wa taifa tamashani.
    B. Sisi tumealikwa kwenda kupanda miti.
    C.Yeye amehudhuria mkutano wa haki za Watoto.
    D.Wao wanatumia vifaa vya kidijitali.

28. Msimu wa baridi kali bila mvua huitwa?
    A. kiangazi
    B. masika
    C. vuli
    D. kipupwe

29. Tegua kitendawili kifuatacho; mwanangu akipigwa watu hucheza
    A. ngozi
    B. ngoma
    C. moto
    D. mawingu

30. Lipi ni jibu sahihi la maagano buriani?
    A. tunayo
    B. dawa
    C. ya kuonana
    D. binuru



Distinction Educational Publishers 2026

## INSHA

*Andika insha ya kusisimua kuhusu:*

**HARUSI YA SHANGAZI**

CamScanner